

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA.

**SHULE YA SEKONDARI DUGA,
S. L. P 2042,
TANGA.
07/12/2020**

Kumb.Na.DGSS/JI/.....

JINA LA MWANAFUNZI:.....

S. L. P......

.....

**YAH: MAAGIZO YA SHULE YA SEKONDARI YA DUGA KIDATO CHA
KWANZA MWAKA 2020.**

1. Ninayo furaha kukuarifu umechaguliwa kujiunga na shule ya secondary ya Duga mwaka 2021 HONGERA SANA
2. Tafadhali soma kwa makini maagizo na kukamilisha mahitaji yanayohitajika shuleni ili uweze kupokelewa na kuanza masomo bila usumbufu.
3. Shule itafunguliwa tarehe 07/01/2021 tafadhali fika bila kukosa kutakuwa na mkutano wa wazazi/walezi wa wanafunzi saa 2:00 asubuhi.
4. Shule ya sekondari ya Duga ni shule ya kutwa, na ni ya mchanganyiko (wavulana na wasichana)

MAAGIZO MUHIMU

- a. Cheti cha Daktari kinachoonyesha kwamba umepimwa vizuri kwenye Hospitali ya serikali (Wialaya, Mkoa) fomu Na.1.
- b. Kukubali nafasi aliyopewa mwanafunzi Fomu Na. 2.
- c. Maelezo binafsi ya mwanafunzi Fomu Na.3.
- d. Sheria za shule Fomu Na.4
- e. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

SERE ZA SHULE

WASICHANA.

- i. Mashati mawili meupe mikono mifupi (Tetrone)
 - ii. (a) Sketi mbili rangi ya kijivujivu iliyoonyeshwa kwenye fomu hii au
- b) Suruali ifanane na kanzu yake ya rangi ya kijivu iliyoonyeshwa kwenye fomu hii au
- (c) Sketi ndefu ifike kwenye nyayo na blauzi ya mikono mirefu na Hijabu kubwa.
- (d) Hijabu isiwe ya mpira iwe ndefu vilivyo.
- (e) Epuka suruali za kubana zitachanwa na utarudishwa nyumbani.
- (f) Sare ya michezo kwa shule hii ni trakisuti nyeusi na tisheti nyeupe ndefu kupita magoti kwa wasichana.

- iii. Viatu vya ngozi nyeusi nyenye visigino vifupi.
- iv. Spksi nyeupe.
- v. Pia beba ndoo ndogo, Fagio na kwa ajili ya kufanyia usafi katika eneo lako ulilopangiwa.

WAVULANA.

- i. Mashati mawili meupe mikono mifupi (tetroni)
- ii. Suruali mbili rangi ya kijivu iliyobandikwa kwenye fomu.
NB: Epuka suruali za kubana zitachanwa na kurudishwa nyumbani
- iii. Viatu vya ngozi jozi mbili nyeusi vyenye kamba.
- iv. Soksi nyeupe.
- v. Bukta nyeuzi na T-shert nyeupe.
- vi. Pia beba ndoo ndogo, Fagio kwa ajili ya kufanya usafi katika eneo lako ulilopangiwa.
NB: Kitambaa kwa ajili ya suruali, Sketi na kanzu kinapatikana shuleni.

TAALUMA

- a. Madaftari makubwa yasiyopungua 11.
- b. Mkebe wa kufanyia Hisabati (Mathematical Set)
- c. Kamusi ya kiingereza.
- d. Kalamu na penseli.

MWISHO

Nakutakia kila la kheri katika maandalizi yako na unakaribishwa shule ya sekondari Duga.

MUHIMU

Kamilisha mahitaji ya shule mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

.....

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI DUGA

MKINGA

NB: MTENGENEZEE KITI NA MEZA MWANAO KUEPUKA KUKAA CHINI.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA.
SHULE YA SEKONDARI DUGA,
S. L. P 2042,
TANGA.**

KANUNI NA SHERIA ZA SHULE.

UTANGULIZI.

Sheria na kanuni hizi ni muhimu zieleweke kuwa ndiyo dira ya salama katika jamii.

1. Sheria za nchi.
Kila mwanafunzi anatakiwa afuate sheria zote za nchi. Ni wajibu kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Fedha ya Taifa nk.
2. Masomo
Shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ni muhimu. Hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule kama ilivyopangwa. Mwanafunzi akifika shuleni anatakiwa kubaki mpaka mwisho wa shughuli za siku.
3. Maadili
 - a. Heshima: Waheshimu waalimu, wafanyakazi, viongozi wa shule, wageni na wanafunzi wenzio hapa shuleni na nje ya shule.
 - b. Usafi wa sare, mwili na mazingira ya shule sharti kuzingatia.
 - c. Ni mwiko kwa wanafunzi
 - Kuvuta sigara, Bangi, Kunywa pombe au kutumia madawa ya kulevya.
 - Kutembela vilabu vya pombe, majumba ya sterehe au majumba ya kufikia wageni.
 - Shule ni mahali pa kusoma na si mahali pa kujipamba hivyo ni marufuku kuchana na kutia dawa yeyote kwenye nywele, kuvyoa mitindo ya kihuni, kupaka rangi kucha au midomo, kuchubua ngozi kwa dawa au kuvaa herein, bangili, pete, mikanda mipana, maandishi kwenye mwili au kwenye mavazi n.k.
4. MIKUTANO NA MAWASILIANO.
 - a. Mikutano na mikusanyiko ya aina yoyote hapa shuleni lazima ijulikane rasmi kwa mkuu wa shule.
5. LUGHA
Lugha inayotumika shuleni ni kiingereza tu isipokuwa wakati wa kipindi cha Kiswahili tu.

TAFADHALI KWA WANAFUNZI

Yafuatayo ni mambo ambayo yanaweza kumfanya mwanafunzi aondolewe katika shule bila maonyo ya awali:

- | | |
|-------------------------|--|
| 1. WIZI | 8. KUPATA/KUTIA MIMBA |
| 2. UASHERATI | 9. KUTOA MIMBA |
| 3. UTORO | 10. KUOA/KUOLEWA |
| 4. ULEVI WA AINA YOYOTE | 11. KOSA LA JINAI KAMA KUVUNJA
SHERIA ZA NCHI |
| 5. KUPIGANA | 12. KUKATAA ADHABU KWA |
| 6. KUGOMA | 13. KUJARIBU MALI AU VIFAA VYA
UMAA MAKUSUDI |
| 7. USHOGA | |

MELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI (PERSONAL PARTICULARS)

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi.

1. Jina kamili la mwanafunzi:.....
2. (a) Trehe ya kuzaliwa
- (b) Sehemu alipozaliwa.....
3. Dini/ Dhehebu
4. Ni raia wa
5. (a) Drasa alilomaliza.....
- (b) Shule aliyomaliza.....
- (c) Anuani ya shule
6. (a) Jina la mzazi
 - i. Mama(Hai/ Amefariki).....
 - ii. Baba(Hai/Amefariki).....

(b) Kazi ya mzazi:

 - i. Baba
 - ii. Mama

(c) Anuani ya mzazi.....

Namba ya simu ya mzazi.....
7. (a) Jina la atakayegharamia mahitaji yako ya shule.....
- (b) Anuani yake ni
- (c) simu yake.....
- (d) Uhusiano..... kama kaka, dada, mjomba n.k.
8. Sehemu utakayoishi
 - (a) (i) Mtaa
 - (ii) Namba ya simu
 - (b) (i) Utaishi na nani?
 - (ii) Una uhusiani gani na huyu uliyemtaja
 - (c) Utaishi na kata ya

SEHEMU HILIJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi..... mzazi/mlezi wa

nakubali ajiunge na shule ya sekondari DUGA na naahidi kumpa vifaa kwa jinsi ilivyoagizwa.

Naahidi nitatimiza na kushirikina na shule kumlea kitabia na kimaadili.

UTHIBITISHO WA AFISA MTENDAJI KATA

Mimi Ambaye ni Afisa Mtendaji Kata ya

..... nathibitisha kwamba kwa kadri ya uwezo wangu, maelezo aliyotoa mwanafunzi katika maelezo binafsi ya mwanafunzi ni y a kweli.

.....

SAHIHI

.....

TAREHE